



# JKT LEO



JARIDA LA MTANDAONI LA JESHI LA KUJENGA TAIFA

TOLEO NA. 179

11 APRILI, 2022

## BURUNDI KUANZISHA JKT - BRIG JEN SIBOMANA



Brigedia Jenerali Ignace Sibomana (wa tatu kushoto mbele) akiwa katika picha ya pamoja na Maafisa Makao Makuu ya Zamani ya JKT pamoja na Ujumbe alioongozana nao kutoka nchini Burundi.

Imetolewa na Kurugenzi ya Habari na Uhusiano,  
Makao Makuu ya Jeshi la Kujenqa Taifa, Sanduku la Posta 2963, Dodoma, Tanzania.  
Simu: +255 26 2962078. Nukushi: +255 26 2962080  
Barua pepe: [info@jkt.go.tz](mailto:info@jkt.go.tz) Tovuti: [www.jkt.go.tz](http://www.jkt.go.tz)

# BURUNDI KUANZISHA JKT- BRIG JEN SIBOMANA

**M**kuu wa Logistiki kutoka Jeshi la Ulinzi wa Taifa la Burundi Brigedia Jenerali Ignace Sibomana amesema Burundi ipo katika mchakato wa kuanzisha chombo cha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) hivyo wamekuja Tanzania kujifunza namna JKT linavyotekeleza majukumu yake toka kuanzishwa kwake.

Brigedia Sibomana ameyasema hayo Makao Makuu ya zamani ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Mlalakuwa Jijini Dar es Salaam Aprili 11, 2022 akiwa na ugeni alioambatana nao na kupata taarifa ya Utendaji kazi wa JKT na Shirika la Uzalishajimali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT).

Ameongeza kuwa, Jeshi la Ulinzi wa Taifa Burundi lina mpango wa kupeleka maombi Katika Serikali yao kuitia Bunge ili mchakato wa kuanzishwa chombo cha namna hii uridhiwe hivyo wamekuja kujifunza.

Ameongeza kuwa, Sio mara ya kwanza kwa nchi hiyo kuja nchini kujifunza kwani hata kuanziashwa kwa kitengo cha Usalama katika Jeshi hilo, Kilitokana na ziara ya kimfunzo waliyofanya hapa nchini mwaka 2015.

Ameishukuru serikali ya Tanzania kwa ushirikiano uliopo baina ya nchi hiyo na kuongeza kuwa Uhusiano huo upo toka miaka 200 iliyopita sawa na karne mbili, Hivyo ameshauriwa uhusiano huo uendelezwe.

Burundi na Tanzania ni Ndugu kwa zaidi ya Karne mbili sasa, Undugu huu ulitokana na Waasisi wa Nchi hizi." Ameongeza

Ameafanua kuwa, Tanzania ndiyo nchi iliyosaidia Burundi kupata Uhuru wake lakini pia imekuwa ikipokea wakimbizi wengi kutoka nchini Burundi kwa kuwa nchi hii ina Amani na wananchi wake wana upendo.

"Sisi kwetu Tanzania ni nyumbani, mmekuwa wakarimu sana kwetu, sisi kwa ujumla wetu tumefurahi sana kufika Tanzania kujifunza mambo mengi ambayo yatatusaidia pia sisi kuanzishwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa nchini kwetu". Amesema Brigedia Jenerali Sibomana

Brigedia Jenerali Sibomana, Ameishukuru pia Uongozi wa JKT kwa mapokezi mazuri toka walipoingia hapa nchini, Pamoja na Taarifa zote zilizowasilishwa kwao.

Naye Kanali Shija Lupi kwa niaba ya Mkuu wa JKT Meja Jenerali Rajabu Mabele, Ameukaribisha tena ugeni huo JKT na kuongeza kuwa Uhusiano huo utaendelezwa sambamba na kuendelea kuenzi historia nzuri iliyowekwa na waasisi wa nchi hizi mbili.

"Ushirikiano baina ya nchi hizi mbili utaendelezwa katika nyanja za Ulinzi, Mafunzo Kubadilishana uzoefu na ujuzi katika masuala ya kijeshi". amesema Kanali Shija Lupi.

Baada ya kutoka Makao Makuu ya JKT ugeni huo pia ulitembelea Mgulani JKT Kiwanda cha Maji (SUMAJKT Bottling Plant) na Kiwanda cha Nguo (SUMAJKT Garment Factory) na kupata fursa ya kujifunza mambo mbalimbali Kikosini hapo juu ya utendaji kazi wa Viwanda hivyo.

Wakiwa Kikosini Mgulani JKT ugeni huo uliweza pia kupata Burudani mbalimbali kutoka katika vikundi vyta Sarakasi, Ngoma za Asili, Bendi ya Kimbunga na muziki wa Steel Band(Mapipa)

Ugeni huo ulivutiwa zaidi na kikundi cha Steel Band na kuahidi kwenda kujipanga ili wasanii wachache kutoka kikundi hicho waweze kwenda nchini Burundi kuwafundisha warundi ngoma hiyo.

Nae Kamanda Kikosi Mgulani JKT Luteni Kanali Ashraf Hassan amesema Kikosi hicho kitaendelea kutekeleza maa-gizo ya Makao Makuu ya JKT kwa kuwapokea vizuri wageni wanaotembelea JKT katika kikosi hicho.

"Sisi kama Wanamgulani tutaendelea kupokea ugeni na kuwa imara katika kuwapokea na kuwakarimu wageni wanaofika Jeshi la Kujenga Taifa ili waweze kujisikia wapo nyumbani kwao na waweze kujifunza nyimbo na utamaduni wetu." ameongeza

Mbali na kutembelea Makao Makuu ya zamani ya JKT ugeni huo utatembelea pia Mgambo JKT na Ruvu JKT mkoani Pwani.



**Brigedia Jenerali Ignace Sibomana akisaini kitabu cha wageni pindi alipowasili Makao Makuu ya JKT mkoani Dar es salaam.**

# MATUKIO KATIKA PICHA

**Brigedia Jenerali Ignace Sibomana kushoto akisalimiana na Mwakilishi wa Mkuu wa JKT Katika Ugeni huo, Kanali Shija Lupi alipowasili Makao Makuu ya JKT mkoani Dar es salaam.**



**Brigedia Jenerali Ignace Sibomana akipokea Salamu ya heshima kutoka kwa Gwaride lililoandaliwa na Jeshi la Kujenga Taifa wakati alipowasili Makao Makuu ya zamani ya Jeshi la Kujenga Taifa Mlalakuwa mkoani Dar es Salaam.**

**Brigedia Jenerali Ignace Sibomana akitagua Gwaride la heshima lililoandaliwa na Kikosi Cha Mgulani JKT mkoani Dar es Salaam.**



# MATUKIO KATIKA PICHA

Mwakilishi wa Mkuu wa JKT,  
Kanali Shija Lupi kushoto  
akimkabidhi zawadi Mkuu  
wa Logistiki kutoka Jeshi la  
Ulinzi wa Taifa nchini  
Burundi Brigedia Jeneral  
Ignace Sibomana kulia pindi  
alipowasili Makao Makuu ya  
JKT mkoani Dar es Salaam.



Brigedia Jeneral Ignace  
Sibomana (kulia) akimkabidhi  
Kanali Shija Lupi zawadi ya  
Mkuu wa JKT ambayo ni  
mfano wa ngao pindi  
alipowasili Makao Makuu ya  
JKT.

Brigedia Jeneral Ignace  
Sibomana ( kushoto) akimpa  
zawadi kutoka nchini Burundi  
Kamanda Kikosi cha Mgulani JKT  
Luteni Kanali Ashraf Hassan.



# MATUKIO KATIKA PICHCHA

Brigedia Jenerali Ignace  
Sibomana akipata Maelezo juu  
ya utendaji kazi wa Kiwanda  
cha Maji kilichopo Mgulani  
JKT.



Brigedia Jenerali Ignace  
Sibomana akipata Maelezo juu  
ya utendaji kazi wa Kiwanda cha  
Nguo kilichopo Mgulani JKT  
mkoani Dar es salaam.

Brigedia Jenerali Ignace  
Sibomana akiwatunza hela kikundi  
cha ngoma katika Ukumbi wa  
Isamuhyo uliopo Mgulani JKT.



# MATUKIO KATIKA PICHA

Brigedia Jenerali Ignace Sibomana (katikati) akiwa Katika picha ya pamoja na Mwakilishi wa Mkuu wa JKT Kanali Shija Lupi, Mwambata Jeshi wa Nchi ya Burundi nchini, Maafisa Wanadhimu wa JKT na ugeni alioongoza-na nao kutoka nchini Burundi.



ISAMUHYO  
HALL



Brigedia Jenerali Ignace Sibomana katikati mbele wa liokaa akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya watendaji wa Kiwanda cha maji Mgulani JKT.

Brigedia Jenerali Ignace Sibomana katikati mbele waliokaa akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya watendaji wa Kiwanda Cha Nguo Mgulani JKT.

